TANGAZO LA SERIKALI Na. 285 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA HIFADHI NA USAFI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA YA MWAKA 2021

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jinan a mwanzo wa Sheria kiutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya mwaka 2021.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa tu kama imeelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hii.

"eneo la Hifadhi" ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji,mbuga za wanyama, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Igunga;

"hifadhi" maana yake ni eneo lolote lililotengwa na Halmashauri au jamii au mtu yeyote kwa lengo la kulifanya eneo hilo kubaki au kurudi katika hali yake ya asili na linajumuisha misitu, mabonde, milima, mabwawa na vyanzo vya maji;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi; mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji unaozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidiniwa chini ya Sheria ya Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"madini ya ujenzi" maana yake ni udongo, kifusi, mchanga, kokoto, mawe na chokaa na vitu vingine vinavyoweza kuchimbwa ardhini kwa kusudi la ujenzi;

"mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004;

"maji taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004;

"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004;

"taka hatarishi au taka hatari" maana yake ni taka katika hali ya yabisi, kimiminika, gesi, au ujiuji mzito, ambazo kwa sababu za mwitikio wake kikemikali, zina madhara kwa afya, maisha au mazingira;

"taka hatari" Maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu,ambayo yanaleta athari za kikemia,kwa binadamu au mazingira;

"taka ngumu" Maana yake ni ile iliyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004;

"Vyanzo vya maji" maana yake ni pamoja na chemchem, mito, mabwawa, ardhi, mabonde ya mito na maeneo ya milima;

"Wakala" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni, au taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri ili kutekeleza majukumu ya Halmashauri kwa mujibu wa

Sheria Ndogo hii.

## SEHEMU YA PILI
## UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kuhifadhi mazingira

3. Utakuwa ni wajibu wa kila mtu ambaye ni mkazi, au mpitaji ndani ya Halmashauri kutunza mazingira.

Upandaji na utunzaji wa miti

4.- (1) Mtu yeyote anayemiliki ardhi atapaswa kupanda miti ya matunda au kivuli isiyopungua minne katika kila eneo la kiwanja chenye ukubwa usiozidi mita za mraba mia nne, na miti isiyopungua kumi kuzunguka shamba lisilozidi eka moja isipokuwa mashamba ya mpunga.

(2) Mtu aliyepanda mti atawajibika kuutunza na kuulinda mti huo na kuhakikisha unakua.

(3) Kila mtu atapaswa kujihepusha kufanya uharibifu kwa mti wowote uliopandwa.

(4) Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria Ndogo hii, kila mtu atakayeharibu mti uliopandwa, atawajibika kupanda upya mti mwingine na kuutunza, na kama sio mkazi, atagharamia upandaji mpya na utunzaji wa mti huo mpaka utakapofikia hatua uliyokuwa umefikia kabla ya kuharibiwa.

Matumizi ya nishati ya kuni

5. Taasisi zote zinazotumia nishati ya kuni kwa matumizi ya kupika zitapaswa kutumia majiko banifu yenye kutumia kuni chache.

Ukataji wa miti

6.- (1) Hakuna mtu atakayekata mti wowote uliopandwa au wa asili katika eneo ambalo halikutengwa kwa ajili ya kukata miti isipokuwa kwa kibali maalum na baada Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa kuona kuna umuhimu wa mti husika kukatwa.

(2) Halmashauri inaweza kutenga maeneo ya misitu ambayo itaruhusiwa kukatwa miti kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

(3) Maombi ya kibali cha kukata mti yatawasilishwa kwa Fomu Na. 1 na kibali kitatolewa katika Fomu Na. 2, zote zinapatikana katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hii.

Taasisi kupanda miti

7. Kila taasisi ndani ya mipaka ya Halmashauri itahakikisha kwamba:-
a) inapanda na kutunza miti katika maeneo yaliyo chini ya uangalizi wake;
b) inashiriki vema katika shughuli za kupanda miti na kuhifadhi mazingira pale watakapotakiwa kufanya hivyo; na

c) inatoa taarifa mara moja kwa Halmashauri au katika ofisi ya kata iliyo karibu, pale inapobainika kuna jaribio lolote la uharibifu wa mazingira ndani ya maeneo yaliyo chini ya uangalizi wa taasisi hiyo au jirani yake.

Wajibu wa Halmashauri katika upandaji na utunzaji wa miti

8. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wengine wa mazingira itakuwa na wajibu wa:-
a) kuanzisha vitalu vya miti na kuhamasisha wadau na wananchi kuotesha miche ya miti ambayo itapandwa katika maeneo mbalimbali ndani ya halmashauri kwa utaratibu utakaopangwa;
b) kutenga eneo kwa ajili ya kupanda miti au kutunza miti iliyokwisha pandwa kama hifadhi ya misitu ambayo hakuna shughuli zozote zitakazoruhusiwa kufanyika katika eneo au maeneo hayo isipokuwa kwa idhini ya Halmashauri;
c) kusimamia utunzaji wa rasilimali za misitu iliyopo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri;
d) kusimamia kampeni za kitaifa, kimkoa na kiwilaya za kupanda miti na kuhifadhi mazingira;
e) kupanga siku moja au zaidi kila mwaka kwa ajili ya kupanda miti ambapo watu wote watakaotakiwa kushiriki katika zoezi hilo watalazimika kushiriki.

Matumizi ya choo

9.- (1) Kila mmiliki wa nyumba ya makazi, au jengo la biashara, ofisi au shughuli nyingine yoyote atapaswa kuwa na choo na kuhakikisha kinatumika ipasavyo.
(2) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kujisaidia vichakani,

maporini, vichochoroni au katika mazingira mengine yoyote isipokuwa chooni.

(3) Kila dereva wa gari la abiria atakuwa na wajibu kuwahamasisha abiria wake kujisaidia katika vyoo vya umma katika maeneo ya stendi au sehemu nyingine zenye huduma ya choo.

Uthibiti wa maji taka

10.- (1) Maji yote yanayotoka chooni, bafuni, yenye mabaki ya chakula yatathibitiwa kikamilifu na mmiliki kiasi cha kutoruhusu kutiririka katika mazingira na kuhatarisha usalama wa mazingira na afya za watu.

(2) Maji taka yote yatahifadhiwa katika mashimo maalum yaliyojengwa kwa saruji na kufunikwa.

(3) Ni marufuku mtu yeyote kumwaga maji taka barabarani.

Uchimbaji wa madini ya ujenzi

11.- (1) Bila kuathiri masharti ya Sheria nyingine, hakuna uchimbaji wa madini ya ujenzi utakaofanyika ndani ya eneo la Halmashauri isipokuwa katika eneo lililotengwa au kuridhiwa na Halmashauri kwa kusudi hilo kwa kuzingati mipango miji, tathimini ya adhari za mazingira na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

(2) Mtu mwenye kibali cha kuchimba madini ya ujenzi ndani ya eneo la Halmashauri kilichotolewa na Wizara ya madini au kwa mujibu wa sheria nyingine, ataruhusiwa kuanza au kuendelea na uchimbaji endapo eneo analotaka kuchimba litakuwa limekaguliwa na Halmashauri na linakidhi masharti ya kifungu kidogo cha (1).

(3) Endapo eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi sio eneo la Halmashauri, mmiliki wa eneo hilo atapaswa kulipa ada ya ukaguzi wa mazingira kwa Halmashauri kwa viwango vilivyobainishwa katika Sheria Ndogo ya ada na ushuru.

(4) Maombi ya kufanyiwa ukaguzi wa mazingira katika eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi yatawasilishwa kwa kutumia Fomu Na. 3

inayopatikana katika Jedwali la kwanza.

(5) Ithibati kuhusu hali ya eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi, ikieleza kama eneo hilo linafaa au halifai kwa shughuli hiyo, itatolewa katika Fomu Na. 4 inayopatikana katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hii.

(6) Bila kujali masharti ya kifungu hiki Halmashauri inaweza kuelekeza ukaguzi wa eneo lolote ili kujiridhisha kama kanuni za utunzaji wa mazingira au masharti ya kibali chochote yanayohusu utunzaji wa mazingira yanazingatiwa.

Viwanda, karakana, gereji na uoshaji wa magari

12.- (1) Shughuli zote za viwanda, karakana, gereji na uoshaji wa magari na vyombo vingine vya usafiri zitafanywa katika maeneo yaliyotengwa na Halmashauri kwa shughuli hizo.

(2) Kila mtu atakayetaka kufanya shughuli mojawapo kati ya zile zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (1), na endapo shughuli hizo zinazalisha maji taka au taka nyingine, mtu huyo atawajibika kuweka miundombinu ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaoweza kusababishwa na shughuli zake.

Uwashaji wa moto

13. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuwasha moto au kufanya jambo ambalo litasababisha moto kuwaka katika sehemu ya kiwanja au shamba au eneo lolote la msitu au pori isipokuwa kwa kibali cha maandishi kutoka Halmashauri.

Utunzaji wa maeneo ya Hifadhi

14.- (1) Maeneo yalioainishwa katika Jedwali La Pili la Sheria Ndogo hii yatajulikana kama maeneo ya Hifadhi.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote, kwanda, taasisi au shirika kufanya shughuli yeyote katika maeneo ya Hifadhi bila kibali cha Halmashauri.

Biashara za mifugo

15.- (1) Biashara zote za mifugo lazima zifanyike katika maeneo yaliyotengwa kwa kusudi hilo.

(2) Kila mfugaji anayepeleka mifugo yake sokoni,

josho, machinjioni au mahali pengine, atapaswa kupitisha mifugo yake katika njia za kupitisha mifugo.

(3) Hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kulima kuweka makazi kwenye njia za kupitisha mifugo.

(4) Kila mfanyabiashara anayetaka kuchinja mifugo yake, atahakikisha mifugo hiyo inachinjwa katika machinjio yaliyoidhinishwa na Halmashauri.

(5) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika eneo lolote kukagua, kudhibiti uchinjaji holela na anaweza kuamuru kuharibiwa kwa mzoga au nyama ambayo haikukaguliwa.

Vituo vya kunenepeshea mifugo

16.- (1) Halmashauri inaweza kuanzisha vituo kwa ajili ya kunenepesha mifugo katika maeneo yanayofaa kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira.

(2) Mtu yeyote anaweza kuanzisha kituo cha kunenepesha mifugo baada ya kupata kibali kutoka Halmashauri.

(3) Kibali cha kuanzisha kituo cha kunenepeshea mifugo kitaombwa kwa barua na kutolewa kwa barua.

Usafirishaji wa mifugo ndani ya Halmashauri

17. Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafirisha mifugo kutoka katika sehemu moja ya Halmashauri kwenda katika sehemu nyingine ndani ya Halmashauri bila ya kuwa na kibali cha maandishi kutoka Halmashauri.

Usafi wa zizi

18. Kila mfugaji atahakikisha zizi linakuwa katika hali ya usafi wakati wote na taka zinaozalishwa kutokana na shughuli za ufugaji zitatupwa au kuhifadhiwa kwa kuzingatia kanuni za afya na usafi wa mazingira.

Kuamisha mifugo

19.- (1) Mkurugenzi anaweza kuamuru mifugo ihamishwe kutoka katika eneo moja kwenda eneo jingine endapo ufugaji katika eneo la kwanza unakinzana na Sheria za mipango miji au ni kero kwa wakazi wa eneo hilo.

(2) Katika zoezi la kuhamisha mifugo chini kifungu

kidogo cha (1), Halmashauri haitahusika na gharama wala hasara ambayo mfugaji anaweza kuipata isipokuwa kama itathibitika hasara imesababishwa na uzembe wa Afisa Mwidhiniwa.

Ukamataji wa mifugo

20.- (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuachia mifugo yake kuzurura ovyo au kuharibu mazao ya mtu mwingine.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukamata mifugo ambayo itakutwa inazurura ovyo, inaharibu mazao ya mtu mwingine au inasafirishwa kutoka eneo moja la Halmashauri kwenda eneo jingine ndani ya Halmashauri bila kibali cha Halmashauri.

(3) Kila mtu ambaye mifugo yake itakamatwa chini ya kifungu kidogo cha (2), atagharamia gharama za ukamataji na utunzaji wa mifugo yake kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(4) Endapo mifugo iliyokamatwa haitakombolewa kwa zaidi ya siku saba kwa kulipiwa gharama za ukamataji na utunzaji, Halmashauri itaipiga mnada mifugo hiyo baada ya kupata amri ya Mahakama.

(5) Fedha itakayopatikana katika mnada chini ya kifungu kidogo cha (4), italipia gharama za ukamataji, utunzaji wa mifugo iliyokamatwa na gharama za mnada na fedha itakayobaki atapewa mmiliki wa mifugo husika.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote inayotokana na kukamatwa kwa mifugo ikiwemo vifo au upotevu isipokuwa pale itakapothibitika kwamba hasara hiyo imesababishwa na uzembe wa Afisa Mwidhiniwa.

Udhibiti wa magonjwa ya mifugo

21.- (1) Kila mfugaji atawajibika kuhakikisha mifugo yake inapata chanjo na matibabu dhidi ya magonjwa ya mifugo kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na Halmashauri.

(2) Halmashauri inaweza kuamuru kuuawa kwa mbwa au mifugo mingine yenye kichaa au inazurura na

ambao kwa maoni ya Afisa Mifugo, ni hatari kwa mazingira au maisha ya binadamu na endapo kuuawa kwa mifugo hiyo kutaonekana ndio njia bora zaidi ya kudhibiti hatari hiyo.

## SEHEMU YA TATU
## USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kutunza na kufanya usafi

22.- (1) Kila mmiliki au mwangalizi wa ardhi, jengo, kaya, kiwanda, ofisi au eneo la biashara, atawajibika kutunza na kufanya usafi katika eneo lake au eneo analolisimamia na mazingira yanayozunguka eneo hilo.

(2) kila mmiliki wa nyumba au eneo au mpangaji ambaye eneo lake linapakana na barabara atawajibika kutunza na kufanya usafi mpaka katikati ya barabara kutoka kwenye mpaka wa eneo lake.

(3) Kila mmiliki au dereva wa chombo cha kusafirishia mizigo atahakikisha anafunika bidhaa anazosafirisha ili kutoruhusu bidhaa hizo kudondoka au kumwagika wakati wa usafirishaji.

(4) Wamiliki au madereva wote wa vyombo vya kusafirisha abiria watahakikisha wanaweka vyombo vya kuhifadhia taka ndani ya magari yao na abiria watawajibika kutumia vyombo hivyo kuweka taka zanazozalishwa ndani ya gari husika.

(5) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka katika maeneo ya wazi, mitaani, barabarani, katika mitaro ya maji ya mvua, vyanzo vya maji na maeneo mengine yasiyoruhusiwa.

Ukusanyaji wa taka ngumu

23.- (1) Kila mmiliki au mpangaji wa nyumba ya makazi au biashara au ofisi, atapaswa kuwa na chombo cha kutunzia taka katika eneo lake na ambacho hakiruhusu taka kuwa wazi au kusambaa.

(2) Utakuwa ni wajibu kwa mwenye nyumba au mpangaji kupeleka taka zake katika kituo kidogo cha kukusanyia taka kilichotengwa na Halmashauri.

(3) Halmashauri inaweza kuweka utaratibu wa kupita nyumba kwa nyumba katika baadhi ya maeneo au maeneo yote kukusanya taka.

(4) Kila mzalishaji wa taka atalazimika kutenganisha taka atakazozalisha kulingana na aina ya taka kwa kuzingatia zile zinazooza, vyuma, plastiki, chupa, karatasi na kuziweka katika vyombo tofauti.

Halmashauri kusafirisha taka ngumu hadi Dampo

24.- (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuzoa taka kutoka katika vituo vidogo vya kukusanyia taka na kuzipeleka katika dampo la Halmashauri.

(2) Endapo Halmashauri itapita nyumba kwa nyumba kukusanya taka, itasafirisha taka hizo moja kwa moja hadi dampo.

Taka hatari

25. Kila mzalishaji wa taka hatari atawajibika kuzihifadhi kwa uangalifu, na kuziteketeza taka hizo katika maeneo yaliyotengwa kwa kusudi hilo.

Ushuru wa taka

26.- (1) Mmiliki wa biashara, mkuu wa kaya, msimamizi wa taasisi au kampuni atawajibika kulipa ushuru wa taka kwa viwango vilivyoelekezwa katika Sheria Ndogo za ada na ushuru za Halmashauri.

(2) Ushuru wa taka wa kila mwezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii utalipwa hadi kufikia tarehe saba ya mwezi unaofuata.

(3) Endapo mtu atatenda kosa linalohusiana na kushindwa kulipa ushuru wa taka, mkosaji ataadhibiwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

27 Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo kuingia katika majengo na maeneo mengine ndani ya muda wa kazi kwa ajili ya kufanya ukaguzi na anaweza kutoa maelekezo kwa mmiliki au msimamizi wa jengo au eneo au mkazi wa jengo husika kuondoa taka au kero nyingine yoyote katika mazingira hayo.

SEHEMU YA NNE
MAMBO MENGINE

Uteuzi wa wakala

28. Halmashauri inaweza kumteua mtu, kampuni, taasisi au kikundi cha kijamii kuwa wakala wa kutekeleza baadhi ya majukumu au majukumu yote ya Halmashauri yaliyobainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Makosa

29.- Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii endapo :-

a) ni mmiliki wa ardhi akishindwa kupanda miti inayotakiwa kupandwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
b) atakata mti bila kibali cha Halmashauri;
c) atashindwa kutunza mti uliopandwa ambao anawajibika kuutunza;
d) akishindwa kujenga na choo bora kwa ajili jengo lake;
e) hatatumia choo na badala yake kujisaidia mahali pengine;
f) ni dereva, akisimamisha gari porini ili abiria wajisaidie porini badala ya kutumia choo;
g) atatiririsha maji taka au maji machafu nje ya mfumo wa maji taka;
h) atafanya shughuli mojawapo kati ya zile zilizoainishwa katika kifungu cha 12 nje ya eneo lililotengwa kwa matumizi hayo;
i) atachoma moto vichaka, shamba, kiwanja au msitu bila kibali cha Halmashauri;
j) atafanya shughuli yoyote katika eneo la Hifadhi bila kibali cha Halmashauri;
k) atafanya shughuli za kilimo, ufugaji, kukata mti, ujenzi au shughuli yoyote ya kibinadamu katika vyanzo vya maji bila kibali cha Halmashauri;
l) atashindwa kulipa ushuru wa kuzao taka;
m) atashindwa kutunza au kufanya usafi katika eneo ambalo anapaswa kufanya au kutunza

usafi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

n) atatupa taka katika eneo tofauti na eneo lililotengwa kwa kusudi hiyo;

o) atakataa kupokea au kusaini uthibitisho wa kupokea hati, taarifa au notisi kwa ajili yake au mtu mwingine ambaye yeye anafanya kazi ofisini kwake au anaishi nyumbani kwake;

p) atachimba madini ya ujenzi katika eneo lililotengwa na Halmashauri bila kibali cha mamlaka husika au bila ithibati inayoonesha kwamba eneo hilo linafaa kwa uchimbaji wa madini ya ujenzi husika;

q) atatoa taarifa za uongo kuhusu jambo lolote linaweza kupelekea kutotekelezeka kwa moja ya masharti ya Sheria Ndogo hii ;

r) atashindwa kwa namna yoyote kutimiza masharti ya Sheria Ndogo hii.

Adhabu

30.- Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii, atalipa faini isiopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja faini na kifungo kwa pamoja.

Uwezo wa kufilililisha kosa

31.- Bila kujali masharti ya Sheria Ndogo hii, Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mtu atakiri kutenda kosa na kuwa tayari kutimiza wajibu wake na kujaza Fomu Na. 5 iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

*Tangazo la Serikali Na. 285 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

Fomu Na. 1
MAOMBI YA KIBALI CHA KUKATA MITI
*(Kifungu cha 6(3))*

1. Jina la Mwombaji...........................................................................................................
2. Anwani ya Mwombaji.....................................................................................................
3. Makusudi ya kukata mti/miti ..........................................................................................
   ..........................................................................................................................................
4. Kiwango cha ukataji unaokusudiwa (kuangusha mti wote au kupunguza matawi)
   .......................................................................................................................................
5. Idadi ya miti inayokusudiwa kukatwa (kuangushwa ............ kupunguza matawi .........)
   ..........................................................................................................................................
6. Ukubwa wa eneo linalokusudiwa kukatwa mti/miti ........................................................
7. Matumizi ya ardhi ambako mti/miti inakusudiwa kukatwa (Kiwanja, shamba, Msitu, mengineyo taja) ............................................................................................................

Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa hapo juu ni kweli tupu na niko tayari kuzingatia masharti ya kibali endapo nitapewa.

Jina la Mwombaji .......................................................................

Saini .............................................................................................

Tarehe ..........................................................................................

*Tangazo la Serikali Na. 285 (Linaendelea.)*

Fomu Na. 2

KIBALI CHA KUKATA MTI/MITI
*(Kifungu cha 6(3)*

1. Jina la Mwombaji ..........................................................................................................
2. Anuani ya Mwombaji ....................................................................................................
3. Sababu ya kutoa/kukataa kutoa kibali ..........................................................................
   .........................................................................................................................................
4. Mahali ambapo kibali hicho kitatumika ............................................................................
   .........................................................................................................................................
5. Idadi ya miti iliyoruhusiwa kukatwa – (kuangushwa......... kupunguzwa matawi...........)
6. Ukubwa wa eneo lililoruhusiwa kukata miti………………………………………..
7. Kibali hiki kitakuwa hai kuanzia tarehe ................. hadi tarehe ...................................

Kimetolewa leo tarehe ............................ mwezi......................mwaka..................................
Jina ....................................................................      Saini .....................................................
Cheo ..................................................................      Tarehe ..................................................
ZINGATIA KWAMBA: Taarifa za uongo za mwombaji zinaweza kupelekea kibali hiki kufutwa na kuchukuliwa hatua nyingine za kisheria.

Fomu Na. 3
MAOMBI YA KUKAGULIWA ENEO LA KUCHIMBA MADINI YA UJENZI
*(Kifungu cha 11(4))*

1. Mimi/Sisi................................................................ wa S.L.P.................. naomba/tunaomba Kukaguliwa eneo langu/letu la kuchimba madini ya ujenzi lililopo (taja mahali eneo lilipo) ............................................................................ ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga.

2. Ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi...............................................

3. Aina ya Madini ya ujenzi yanayokusudiwa kuchimbwa katika eneo linaloombewa ukaguzi ni mawe/kokoto/kifusi/mchanga/chokaa/udongo/mengineyo yataje ............................................

Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa ni kweli tupu na niko tayari kuzingatia masharti ya kibali endapo nitapewa kibali hicho.

Jina la Mwombaji .........................................................................
Saini ............................................................................................
Tarehe ..........................................................................................

Fomu Na. 4

ITHIBATI YA HALI YA MAZINGIRA KATIKA ENEO LINALOKUSUDIWA KUCHIMBWA MADINI YA UJENZI

*(Kifungu cha 11(5))*

A. *Taarifa za Msingi:*

1. Jina la mwombaji wa ukaguzi..........................................................................................
2. Anwani ya makazi ya mwombaji……………………………………………………………..
3. Mahali eneo linalokusudiwa kuchimba madini ya ujenzi lilipo………………………………
    i. Kitongoji/Kijiji………………………………………………………………..……
    ii. Kata……………………………………………………………………..………
    …….
4. Ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi……………………………..
5. Aina ya madini ya ujenzi yanayokusudiwa kuchimbwa katika eneo hilo …………………..

B. *Ukaguzi na Mapendekezo*

6. Tarehe ya Ukaguzi wa Mazingira ya eneo la uchimbaji…………………………………
7. Eneo linafaa/halifai kuchimbwa madini ya ujenzi tajwa kwa sababu..........................................................................................................................………
8. Mwombaji aruhusiwe/asiruhusiwe kuchimba madini ya ujenzi katika eneo hilo kwa sababu
    ...................................................................................................................................

*Endapo eneo linalofaa kuchimbwa madini ya ujenzi, mmiliki anaelekezwa kupanda miti na kuhakikisha miti hiyo inakua katika eneo lote atakalokuwa amechimba madini ya ujenzi kwa uwiano wa miti isiyopungua therathini kwa ekari mara baada ya uchimbaji.*

| | |
|---|---|
| Saini ............................................... | Saini ....................................................... |
| Jina ................................................. | Jina .......................................................... |
| Tarehe ............................................ | Tarehe ..................................................... |
| Afisa Mazingira wa Halmashauri | Afisa Mipango Miji/Ardhi wa Halmashauri |

Imethibitishwa

Saini ............................................
Jina .............................................
Tarehe ........................................
Cheo: Mkurugenzi wa Halmashauri

JEDWALI LA PILI

SEHEMU YA I
MAENEO YA HIFADHI
(Kifungu cha 14(1))

Maeneo yafuatayo yatajulikana kama maeneo ya Hifadhi na hakuna shughuli za kibinadamu zitakazofanyika katika maeneo hayo bila idhini ya maandishi ya halmashauri:

i. Bonde la Wembele.
ii. Tindiga la Bulenya.
iii. Mitelemko inayoingiza maji bwawani na bwawa lenyewe la Mwamapuli.
iv. Misitu ya mlima Bulenya, msitu ya Igoweko, msitu wa Uswaya, msitu wa Mwamaganga, msitu wa Unyambiu na msitu wa kijiji cha Mgazi.

SEHEMU YA II
GHARAMA ZA UKAMATAJI NA UTUNZAJI WA MIFUGO
(Kifungu cha 20(3))

| Na | Aina ya Mifugo | Gharama za Ukamataji Wa Mifugo (TSHS) | Gharama za Utunzaji wa Kila Mfugo kwa Siku(TSHS) |
|---|---|---|---|
| | Ng'ombe | 5,000/= | 10,000/= |
| | Punda | 5,000/= | 10,000/= |
| | Nguruwe | 5,000/= | 10,000/= |
| | Ngamia | 5,000/= | 10,000/= |
| | Mbuzi au kondoo | 2,000/= | 5,000/= |
| | Kuku au Bata | 500/= | 1,000/= |
| | Mifugo mingine isiyotajwa | 2,000/= | 5,000/= |

JEDWALI LA TATU

*(Imetungwa Chini ya kifungu cha 31)*

KUFILILISHA KOSA

Mimi……………………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kwamba Tarehe ………Mwezi………..Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya mwaka 2021.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi ninachodaiwa pamoja na faini na kutekeleza wajibu niliopewa na Sheria Ndogo hii.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………. ya Mwezi……………….………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini……………………………………Tarehe…………………………………

*Tangazo la Serikali Na. 285 (Linaendelea.)*

Nembo na Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga vimebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika 3/4/2020 na ubandikaji huo kushuhudiwa na:-

REVOCATUS L. K. KUULI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Igunga*

PETER ONESMO MALODA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Igunga*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma, SELEMANI SAID JAFO (MB.),
22 Februari, 2021 *Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*